MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

TMA TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.11. Msimu wa Kilimo 2023/24* *Tathmini ya Januari 11-20, 2024 na Matazamio kwa Kipindi cha Januari 21-31, 2024*

**MUHTASARI**

- Hali ya mazao na malisho katika maeneo mengi nchini ni nzuri.
- Mvua zinazotarajiwa katika maeneo mengi nchini zitasaidia ukuaji wa malisho na mazao .
- Wakulima na wafugaji wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao na mashamba ili kuweza kukabiliana na athari mbalimbali zinazoweza kujitokeza

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2024


Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) ilipungua nguvu wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliimarika. Hali hii iliendelea kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kuwepo katika baadhi ya maeneo ya kusini nchini.

Kwa upande mwingine hali ya joto la bahari la juu ya wastani liilikuwepo katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hasa katika eneo la mashariki mwa kisiwa cha Madagascar lilichangia katika kutengenezwa kwa migandamizo midogo ya hewa katika eneo hilo. Migandamizo hiyo midogo ya hewa ilipelekea kuvutwa kwa hewa kutoka kaskazini magharibi (Misitu ya Congo) kupitia maeneo ya magharibi mwa nchi na yale ya ukanda wa pwani. Hali hii ilisababisha kuletwa kwa unyevunyevu kutoka misitu ya Congo na hivyo kuchangia kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo.

Viashiria vya hali ya hewa tajwa hapo juu vilipelekea baadhi ya maeneo ya nchi yetu kupata vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi hususan katika maeneo ya kusini, nyanda za juu kusini magharibi, ukanda wote wa pwani na magharibi mwa nchi. Hata hivyo, maeneo mengine ya nchi yalipata vipindi vya mvua nyepesi hadi za wastani katika maeneo machache.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2024

Katika kipindi hiki, maeneo mengi nchini yalipata mvua kati ya milimita (mm) 11 hadi 150 na maeneo machache yaliyosalia yalipata jumla ya mvua kwa siku kumi kiasi cha zaidi ya milimita 200 hususan katika mikoa ya Morogoro na Pwani kama inavyoonekana katiaka Kielelezo.




Kielelezo 1: Kiasi cha mvua kwa siku 10 kwa kipindi cha Januari 11-20, 2024

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2024

Katika dikadi hii, mvua zilizonyesha katika maeneo mengi nchini zilisaidia ukuaji na maendeleo ya mazao.
Maeneo yanayopata mvua za vuli, mahindi yapo katika hatua ya kubeba na kukomaa. Hata hivyo, mvua ya mawe iliyoambatana na upepo iliathiri mazazo ikiwemo migomba ya ndizi hususan katika mkoa wa Kilimnjaro. Pia zao laa maharagwe ambalo lipo katika hatua ya kukomaa katika mikoa ya Kagera,Mwanza na Kilimanjaro limeathiriwa na hali ya mvua katika maeneo hayo.

Mahindi katika maeneo yanayopata mvua za Msimu yapo katika hatua ya ukuaji isipokuwa katika mikoa ya Kigoma na Tabora ambako mahindi yapo katika hatua ya kutoa mbelewele na kubeba. Viazi mviringo vipo katika hatua ya kutoa maua katika mkoa Njombe.

Kwa maeneo yanayolima mpunga hususan katika maeneo ya mikoa ya Tabora, Mbeya, Rukwa na Morogoro, wakulima waliendelea na shughuli za upandaji wa zao hilo.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyama umeendelea kuimarika nchini.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 11-20, 2024

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mabonde vimeongezeka kidogo kutokana na mvua zinazoendelea.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31,2024

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuimarika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kuwepo katika baadhi ya maeneo ya kusini mwa nchi.

Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi, hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha kutengenezwa kwa migandamizo midogo ya hewa baharini na hivyo kuvuta upepo kutoka kaskazini magharibi kupitia nchini na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31,2024

Maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) yanatarajiwa kuwa na mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Mikoa ya magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kuwa na mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani, na Dar es Salaam vikiwemo visiwa vya Unguja na Pemba) inatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) inatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro) zinatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo mengi.

Pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) zinatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo mengi.

Maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua katika maeneo machache.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31,2024

Mvua zinazotarajiwa katika maeneo mengi nchini zitasaidia kuongeza unyevunyevu katika udongo ambao utasaidia katika ukuaji na maendeleo ya mazao. Hata hivyo, mvua hizo zikiwa nyingi zinaweza kuathiri ukuaji wa mazao.

Wakulima wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao ili kuweza kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na unyevunyevu wa udongo wa kupitiliza, kutuama kwa maji kwa mashamba yaliyoko mabondeni, na milipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea pale vitakapojitokeza. Aidha, ukaushaji wa mazao, palizi na matumizi ya pembejeo vinatarajiwa kuathirika kutokana na vipindi vingi vya mvua na unyevu wa kupitiliza.

Wavuvi wanashauriwa kuimarisha miundombinu ya ufugaji wa samaki, na kuchukua tahadhari kwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye bahari ya Hindi na Maziwa Makuu ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi ili kuepuka athari zitokanazo na upepo mkali na mvua kubwa pale vinapojitokeza.
Wafugaji wanashauriwa kupanda majani ya kutosha na kuchimba mabwawa ya kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA JANUARI 21-31,2024

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka kutokana na mvua zinazoendelea. Jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadaye.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)